# Edulog Parent Portal yenye Maeneo ya Mabasi kwa GPS

Mwongozo wa Marejeleo wa Hatua kwa Hatua

## Hatua ya 1  Sakinisha Programu

Tafuta programu ya Edulog Parent Portal katika Google Play Store au iOS App Store, na uisakinishe. Tafuta aikoni ya Edulog yenye rangi ya samawati-kijani. Unaweza pia kutumia msimbo wa QR uliotolewa katika Hatua ya 2.



## Hatua ya 2  Jisajili

Changanua msimbo wa QR kwa kutumia simu yako ya kisasa ili kusakinisha programu ya Edulog Parent Portal. Baada ya programu kusakinishwa, gusa "Sign Up" kwenye Skrini ya Kuingia. Chagua "Tap Here" ikiwa wilaya yako ya shule imekuagiza uingie kupitia mtoa huduma wa wilaya yako.



### Hatua ya 3 Usajili

Weka Jina lako la Kwanza na Jina lako la Mwisho. Ingiza Barua yako Pepe. Ingiza na Uthibitishe Nenosiri. Kisha gusa kwenye "Sign Up."



## Hatua ya 4  Washa Arifa

Kuruhusu arifa kutakuwa muhimu ili kupokea mawasiliano kutoka kwa programu. Hii inaweza kubadilishwa wakati wowote katika mipangilio ya simu yako.



## Hatua ya 5  Uthibitishaji

Utapokea ujumbe: Usajili umefanikiwa! Tafadhali angalia barua pepe kutoka kwa no-reply@edulog.com ili kuthibitisha anwani yako ya barua pepe.

## Hatua ya 6  Ingia

Ingiza barua pepe yako. Ingiza nenosiri lako. Chagua "Sign In".



### Hatua ya 7  Wanafunzi

Usafiri wa Wanafunzi haujaorodheshwa bado. Nenda kwenye "Student List" katika menyu iliyo chini ya programu.



## Hatua ya 8  Ongeza Mwanafunzi

Gusa ADD STUDENT ili kuomba ufikiaji kwa data ya mwanafunzi wako.



### Hatua ya 9  Tafuta Shule

Anza kuandika jina la shule ya mwanafunzi au uitafute kwa kutumia kitufe cha FIND SCHOOL ON MAP.



## Hatua ya 10  Thibitisha Shule

Kisha uthibitishe kwamba umechagua shule sahihi kutoka kwenye wilaya yako ya shule.



### Hatua ya 11  Ongeza Taarifa za Mwanafunzi

Ingiza taarifa zinazoombwa, ambazo zinaweza kujumuisha jina la mwanafunzi, Kitambulisho cha Mwanafunzi, na Tarehe ya Kuzaliwa. Baadhi ya wilaya za shule zinatumia msimbo wa kipekee wa Ombi la Kufikia Taarifa za Mwanafunzi (SAR). Kisha bonyeza "Done."






## Hatua ya 12  Idhini

Mwanafunzi ataonyeshwa kama Approved. Ikiwa ataonyeshwa kama "Pending", taarifa ulizoingiza hazikulingana. Ili kujaribu tena, telezesha kidole kuelekea kushoto kwenye jina la mwanafunzi ili kufuta ombi hili. Gusa jina la mwanafunzi ili kuona Taarifa za Mwanafunzi.



## Hatua ya 13  Maelezo ya Mwanafunzi

Unapochagua jina la mwanafunzi kutoka kwenye orodha ya wanafunzi, taarifa za maelezo ya mwanafunzi zitaonyeshwa. Ili kuona taarifa za basi, gusa "Where's My Bus".



## Hatua ya 14  Basi Langu Liko Wapi?

Shule, kituo kinachofuata cha basi, na basi vitaonyeshwa kwenye ramani, taarifa za safari zikiwa chini yake. Ili kurudi nyuma, chagua mshale wa kurudi nyuma. Muhuri wa muda unaonyesha wakati basi hili liliporipoti eneo lake la mwisho kupitia GPS. Wilaya ya shule inaweza kuweka mipaka ya iwapo na wakati eneo la basi litaonyeshwa.



## Hatua ya 15  Taarifa za Mwanafunzi — Ratiba ya Usafiri

Ili kuona eneo la kituo cha basi na nyakati zilizopangwa, chagua "Transportation Schedule".



## Hatua ya 16  Ratiba ya Usafiri

Unapoachagua Transportation Schedule, kutaonyeshwa muda wa Kuchukuliwa Kwenda Shuleni na muda wa kushushwa Kutoka Shuleni. Chagua mojawapo ya vigae ili kuona maelezo zaidi.



### Hatua ya 17  Mipangilio ya Arifa — Kwenda Shuleni na Kutoka Shuleni

Unaweza kuchagua wakati ungependa kupokea arifa za kuwasili kwa basi. Wazazi wengi huchagua "Pick-Up" kwa safari ya Kwenda Shuleni na "Drop-Off" kwa ziara ya Kutoka Shuleni. Baadhi ya wazazi huchagua kupokea arifa wakati basi linakaribia shule kwa safari ya Kwenda Shuleni. Kumbuka: Huenda arifa ya "Pick-Up" katika shule kwa safari ya Kutoka Shuleni isipatikane kwa wilaya ya shule yako.






### Hatua ya 18a  Maeneo ya Tahadhari — Muhtasari

Ili kubadilisha mipangilio ya arifa, chagua aikoni ya kengele. Hapa ndipo unapoweza kuweka muda, umbali, na katikati ya eneo lako la tahadhari.



## Hatua ya 18b  Maeneo ya Tahadhari — Hariri Eneo la Tahadhari

Weka muda, umbali, na katikati ya eneo lako la tahadhari kwa kutumia skrini ya Edit Alert Zone ‘Kuhariri Eneo la Tahadhari’.



### Hatua ya 18c  Maeneo ya Tahadhari — Sogeza Katikati

Unaweza kusogeza KATIKATI ya eneo lako tahadhari la CIRCLE kwa kugusa kwenye skrini, kisha "Save".



### Hatua ya 18d  Maeneo ya Tahadhari — Rekebisha Ukubwa

Unapochagua Circle, unaweza pia kurekebisha ukubwa wake. Baada ya kuweka katikati na ukubwa wa eneo la tahadhari la mduara, unaweza kulibadilisha kuwa eneo la tahadhari lenye umbo la poligoni lenye ncha 3, 4, 5 au 6.



## Hatua ya 18e  Maeneo ya Tahadhari — Umbo la Poligoni

Unapochagua "Polygon", unaweza kuchagua eneo lenye pande 3, 4, 5 au 6. Unaweza kusogeza ncha (nodi) za kibinafsi ili kubinafsisha umbo la eneo la tahadhari na kuyajumuisha baadhi ya maeneo unayotaka na kuyaondoa mengine. Bonyeza ncha ya nodi kwa sekunde moja au mbili, kisha uisogeze hadi eneo unalotaka na uchague "Save".






### Hatua ya 18f  Maeneo ya Tahadhari — Weka Muda wa Tahadhari

Baada ya kuweka mduara na ukubwa wa Eneo la Tahadhari, weka muda wa Tahadhari kwa kwa kugusa kwenye "Alert in". Arifa hutumwa tu wakati ndani ya kipindi hiki cha muda.



## Hatua ya 18g Maeneo ya Tahadhari — Thibitisha na Hifadhi

Chagua Muda wa Kuanza na Muda wa Kumaliza ambao utapokea arifa kwamba basi limeingia kwenye Eneo. Kisha chagua "Done". Hakikisha umechagua "Save" ili kuhifadhi Eneo la Tahadhari.






## Hatua ya 19  Mipangilio

Katika menyu kuu, gusa kwenye "Settings." Hapa unaweza kubadilisha nenosiri lako, kuweka arifa, kuchagua lugha yako, kuchagua vipimo na kuangalia masasisho.



## Hatua ya 20  Badilisha Nenosiri

Chagua “Change Password” katika  Settings ili kubadilisha nenosiri lako na uguse "Submit". Kisha angalia barua pepe yako kutoka support@edulog.com.



## Hatua ya 21 Arifa

Washa arifa kwa kugusa kwenye kitufe cha kutelezesha. Hii itakupeleka kwenye mipangilio ya arifa ya simu yako.




## Hatua ya 22  Maeneo ya Tahadhari ya Safari

Unapochagua Arifa za Maeneo ya Tahadhari ya Safari, unaweza kuona kila Ukubwa wa Eneo la Tahadhari. Chagua ">" ili kurekebisha.

### Hatua ya 23  Lugha

Gusa kwenye "Language" katika Mipangilio ili kuchagua kugha yako kisha uguse "Save".



### Hatua ya 24  Vipimo

Unapochagua " Units" kwenye skrini ya Mipangilio, unaweza kuchagua Maili au Kilomita, kisha kuchagua "Save". Ili kurudi kwenye menyu kuu, chagua mshale wa kurudi nyuma. Kisha chagua "Home".



## Hatua ya 25  Nyumbani

Kwenye kichupo cha Home utaona maelezo ya safari zijazo. Rangi ya pinki inaonyesha kwamba basi liko karibu. Pia utapata Kisanduku ambapo ndani yake arifa na ujumbe wako huhifadhiwa.



### Step 26  Nyumbani — Kisanduku cha Ndani

Kisanduku chako cha Ndani “In Box” huhifadhi arifa zinazopokelewa kwenye programu. Kulingana na utekelezaji wa wilaya yako, hii inajumuisha taarifa za kuwasili kwa mabasi, mabadiliko ya usafiri, na ujumbe kutoka kwa idara ya usafiri.

